

Alex Tarimo alifanya kazi ya ualimu akifundisha somo la Uchumi kuanzia mwaka 1997 – 2005 katika Shule za Sekondari za Tegeta, White Lake na Feza zote za Dar es Salaam. Aliajiriwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama Afisa Elimu mwaka 2006 na alifanya kazi katika Shule za Sekondari za Galanos (Tanga) na Pugu (Dar es Salaam). Mwaka 2007 alihamia Wizara ya Maji kama Mchumi II na tangu hapo amepanda madaraja mbalimbali hadi kufikia daraja la Mchumi Mkuu. Katika Wizara ya Maji anafanya kazi zinazohusu Sera, Mipango, Bajeti pamoja na Ufuatiliaji na Tathimini ya miradi.

Bw. Tarimo alizaliwa Wilayani Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro mwaka 1969. Alipata Elimu ya Msingi katika Shule ya Msingi Kunduchi, Dar es Salaam (1979 – 1985), Elimu za Sekondari katika Shule za Azania, Dar es Salaam (1986 – 1989) na Ndanda, Mtwara (1990 – 1992). Alipata Shahada ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (1997), Shahada ya Uzamili (MBA) kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (2008), na Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Uwekezaji (*Msc Investment Management*) kutoka Chuo Kikuu cha Coventry nchini Uingereza (2016). Aidha, ana Stashahada ya Uzamili ya Ualimu (*PGDE*) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (2011) na mbobezi katika masuala ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binasfi (*Certified Public Private Partnership Specialist*), elimu aliyoipata kutoka *IP3 College*, Washington, Marekani (2012).

Aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Msaidizi katika Idara ya Sera na Mipango mwaka 2020.